

# UTUREHEMU EE BWANA

Felician Luhenga

YKM - Sengerema

10.02.2024

*Moderato*

U tu re he mu Ee Bwa na (Bwa na) kwa ku wa tu me te nda dha mbi.

Ee Mungu, unirehemu sawasawa na fadhili za - ko, Kiasi cha wingi wa rehema zako uyaafute makosa ya - ngu,

Unioshe kabisa uovu wangu, unitakase dha - mbi za - ngu.

2. Maana nimejua mimi makosa yangu,  
Na dhambi yangu i mbele yangu da i - ma/  
Nimekutenda dhambi wewe peke ya - ko/  
Na kufanya maovu mbele za ma-cho ya - ko.

3. Ee Mungu, uniumbie moyo safi,  
Uifanye upya roho iliyotulia ndani ya - ngu/  
Usinitenge na uso wa - ko/  
Wala roho wako mtakatifu usini - o - ndo - le - e.

4. Unirudishie furaha ya wokovu wako;  
Unitegemeze kwa roho ya we pe - si/  
Ee Bwana, uifumbue midomo ya - ngu/  
Na kinywa changu kitazinena si - fa za - ko.